INTERNATIONAL JOURNAL OF SOCIAL Sciences and Information Technology
ISSN 2412-0294 www.ijssit.com
http:// www.ijssit.com

# DHULUMA KAMA KICHOCHEO CHA MZINDUKO WA WANAWAKE KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI

[1*] **Lucy A. Mboya**
*lucyatieno9@gmail.com*

[2**] **Sangai Mohochi**
*mohochis@ruc.ac.ke*

[3***] **Simiyu Kisurulia**
*kisurulia@yahoo.com*

**Ikisiri**

*Kwa kipindi kirefu wanawake wametwezwa na kudunishwa kutokana na dhuluma wanazofanyiwa na jamii inayotawaliwa na mfumo wa kuumeni. Dhuluma wanazopata wanawake zinatokana na asasi tofauti tofauti ambazo ndizo zinapaswa kudumisha mshikamano wa kijamii. Tahakiki na tafiti nyingi zinaonyesha athari ya ukandamizaji wa jinsia ya kike na hali ya kuzimwa kwa juhudi zake katika kupigania nafasi yake. Mwanamke anavyoitikia hali hii kwa njia inayomzindua na kumfaidi ni suala ambalo halijaangaziwa pakubwa. Ni kutokana na msingi huu ambapo makala hii inachunguza namna dhuluma wanazopata wanawake zinavyowazindua na kuwapa motisha ya kujikomboa na kujinasua kutokana na hali hii ya kusakamwa na asasi kandamizi za kijamii. Kwa njia hii, wanawake wanapata nafasi ya kujiendeleza katika nyanja mbalimbali ikiwemo kujieleza kimapenzi badala ya kuridhia kuishi vivulini mwa waume zao dhalimu. Hali hii inampa mwanamke taswira mpya kama kiumbe mwenye thamani na mchango mkubwa katika kuongoza juhudi za ufanisi wa jamii yake. Uchunguzi huu umeegemea fasihi andishi ya Kiafrika kwa kurejelea kazi mbili: Nyuso za Mwanamke (Mohamed, 2010) na Heri Subira (Babu, 2010). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa kimakusudi. Riwaya hizi zimesheheni hali ngumu ya maisha wanayopitia wahusika wa kike hasa katika harakati zao za kujinasua kiuchumi na kujisaka kimapenzi. Aidha zimeangazia masuala ya wanawake kwa uangavu na kwa namna inayopanua nafasi ya jinsia ya kike katika dunia ya kisasa. Kutokana na mchango mkubwa wa wanawake katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa jamii, ni bayana kuwa matumizi ya fasihi kama wenzo wa kuwazindua wanawake kijamii ni hatua muhimu katika maendeleo ya jamii.*

## 1.0 Utangulizi

Jamii nyingi za Kiafrika zinazotawaliwa na ubabedume zimemsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu kinachodhulumiwa na kufungiwa katika ngome ya utegemezi na uhitaji. Mwanamke ameumbiwa dunia yake maalum katika jamii ambapo anasawiriwa kuwa ni kiumbe duni. Asasi tofauti tofauti kama vile ndoa na dini, ambazo ndizo zinapaswa kudumisha mshikamano wa kijamii, zimemtenga kitamaduni, kisiasa na kiuchumi na kumuumbia dunia yake anamoishi katika upweke na uhitaji. Hynes (1989) anasema kwamba wanawake wamenyang'anywa uwezo wa kujiendeleza na kufanya uvumbuzi. Hivyo basi wamepoteza nafasi ya kushiriki katika maendeleo ya kiteknolojia kama anavyoshiriki mwanamume**.**

Kadiri jamii inavyoendelea ndivyo mwanamke naye ametambua hali yake duni na kuanza kutafuta njia za kujinusuru kutoka katika hali hii. Mabadiliko haya ambayo yameonekana katika jamii yamejitokeza pia katika fasihi andishi ya Kiswahili na ndiposa katika karatasi hii tunaangalia namna suala hili la kutumia dhuluma kama wenzo wa kujikomboa kwa mwanamke limeangaziwa na waandishi wa fasihi ya Kiswahili.

## 2.0 Dhuluma dhidi ya Wanawake katika Fasihi

Kama inavyodhihirika katika kazi za fasihi, wanawake wanapitia aina tofauti za dhuluma katika jamii wanamoishi. Wasomi na wahakiki wa kazi za fasihi wameshughulikia suala la dhuluma kwa wanawake na athari zake kwa muda mrefu bila kutoa suluhu. Kazi tofauti tofauti za fasihi zinaonyesha kuwa juhudi za wanawake katika kupigania ukombozi wao hazijafua dafu kwani juhudi zao aghalabu huonekana kuzimwa na nguvu za asasi za kijamii.

Tafiti za wasomi kama vile Kimani (2003), Rai (2003), Freeman (1975), Momanyi (1998), Wegesa (1994), Lugano (1985 na 1998), Rowbotham (1992), Corrin (1996), Matteru (1992), Welchman (2007), Disch (2009), Mbogo (1992), Corrin (1984), Muindi (1990) miongoni mwa wengine zimeonyesha kuwa mwanamke amedhulumiwa kwa kupigwa, kutawishwa, kutukanwa, kuozwa bila hiari, kubakwa na kadhalika. Wengine wamedharauliwa na hata kukataliwa na wazazi. Dhuluma hizi zimewaathari wanawake kwa njia mbalimbali kama vile ndoa zao kuvunjika, kuhuzunika, kukumbwa na upweke, kuasi, na pia kuingiwa na fikra za kulipiza kisasi.

Hata hivyo, baadhi ya wanawake wamejitokeza kukabiliana na hali hii. Wanawake hawa wametambua kwamba wana haki na uwezo sawa na wanaume katika masuala ya kijamii. Mwanamke wa kisasa anaonekana kudai nafasi yake katika jamii kwa kutumia hali ngumu inayomkabili kama ngazi ya kukwea kwenye ufanisi. Hivi ni kusema kuwa ukandamizaji huwa na athari chanya unapowazindua wanawake na kuwafanya wapige hatua kiuchumi pamoja na kufanya uamuzi ufaao kuhusu suala la mapenzi na ndoa.

Makala hii imeegemea nadharia ya ufeministi. Nadharia ya ufeministi inaangalia na kujaribu kupendekeza suluhu kwa matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Katika karne ya kumi na tisa, vuguvugu la kifeministi lilianzishwa na wanawake walioanza kupigania demokrasia kudai kwamba wao pia wana haki ya kuchangia mabadiliko ya jamii na uwezo wa kuzajisha mali na kumiliki rasilmali kama walivyo wanaume. Wanawake walianza kupigania demokrasia katika siasa pamoja na haki zao katika umiliki wa rasilimali.

Nadharia ya Ufeministi iliasisiwa na Wollstonecraft (1792) kama njia ya kuangalia uwezekano wa kuwepo kwa mwanamke mpya ambaye anaweza kubadilisha jamii kwa kupendekeza suluhu kwa matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Greer (1971) anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa huwafanya kumilikiwa, kudhibitiwa na kukoseshwa uhuru wao. Hivyo basi baadhi ya wanaufeministi wanapendekeza njia za kiharakati kama suluhu kwa matatizo yanayomkumba mwanamke. Hata hivyo, huu si mtazamo pekee kwani wanaufeministi wengine wanapendekeza suluhu za amani zinazosisitiza kuelewa hali aliyomo mwanamke na juhudi kufanywa ili hali hii iboreshwe.

## 3.0 Mzinduko wa Wanawake Dhidi ya Dhuluma

Dhuluma ni tendo la kumnyanyasa mtu kwa kumnyima haki zake, kumdunisha pamoja na kumtendea ukatili. Sehemu hii inamulika mzinduko wa wanawake kutokana na dhuluma wanazokumbana nazo katika riwaya mbili zilizotumika katika uchunguzi huu.

### 3.1 Mzinduko wa Kiuchumi

Mzinduko wa kiuchumi unajitokeza pale mwanamke anapojikakamua na kujiinua kiuchumi ili ajitegemee. Katika *Nyuso za Mwanamke* (2010), Bimkubwa anastahabu kulala njaa na kupiga mafunda ya maji almuradi ahifadhi mijipesa ambayo mchumbawe (mpenziwe aliyetenganishwa naye) Faisal, alimtumia kila mwezi ili

kumfaa bintiye Nana baadaye. Bimkubwa anaiweka akiba ya pesa hizi kwenye benki hadi inafika shilingi milioni tisini. Mijipesa inageuka kuwa kiasi kikubwa cha pesa ambazo anamkabidhi bintiye Nana. Nana anazipokea pesa hizi kama urithi kutoka kwa marehemu mamake. Anaimarika kiuchumi. Bimkubwa anamtengenezea Nana msingi wa kujitegemea katika maisha yake ya baadaye. Waaidha, Bimkubwa anatambua kuwa mwanamke hawezi kuwa huru iwapo hana msingi wa kujitegemea. Haya yanadhihirika katika Nyuso za Mwanamke (uk.172).

Bimkubwa anatambua umuhimu wa uwezo wa kiuchumi kwa mwanamke. Vilevile anatambua kwamba hali ya utegemezi wa wanawake kwa wanaume huchangia katika kudhulumiwa kwao. Mwanamke hana sauti ya kujitetea kwa kuwa mahitaji yake yote yanakidhiwa na mwanamume. Bimkubwa anampa Nana matumaini ya kuanza kujitegemea na kuanzisha miradi ya maendeleo. Bimkubwa anadhihirisha mzinduko wake kwa namna anavyoona mambo kwa njia tofauti.

Kwa upande mwingine, Nana anatambua kwamba kule kunyanyaswa kwa mwanamke kunatokana na tamaduni kandamizi. Anakataa dhuluma alizofanyiwa na babake kwa kupigwa, kutawishwa pamoja na jaribio la babake la kumuoza kwa mtu asiyempenda. Anaonyesha kwamba hataki ukandamizaji wa wanawake anaposema kwamba, licha ya kutotaka kubaki jikoni kupika na kupakua, kuosha vyombo, kufagia na kutunza watoto, hataki kamwe hata kuwa mwanamke kwa maana ya mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamme kama mamake wa kambo, au mwanamke hohehahe anayefyonzwa damu taratibu huku akimalizika kama alivyomalizika mamake mzazi (uk.107-108). Nadharia ya ufeministi inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali na thamani ya binadamu.

Nana anaendelea kuonyesha msimamo wake anaposema kwamba akifumbua macho kutazama kila upande ndani ya jamii yake, huchukia mno tabia ya mwanamke kuwa mwanamke kwa namna mbalimbali zinazopangwa na mwanamume (uk.108). Nana anaamini kwamba ni jukumu la mwanamke kujitokeza ili kupigana na ukandamizaji anaofanyiwa. Anasema:

> Sikukuzwa kibarubaru ili niwe mwanamke wa kudanganyia. Nilizaliwa mwanamke nikakuzwa mwanamke – tena mbali na mamangu. Kwa hivyo nilihisi lazima nipigane mwenyewe kuwa mwanamume katika macho ya watu wanaoniona mwanamke (uk.108).

Nana amezinduka, amepevuka. Yuko tayari kupigania nafasi yake machoni mwa wale wanaomdharau kwa msingi wa jinsia yake ya kike. Lengo lake ni kuuonyesha ulimwengu kwamba mwanamke anao uwezo wa kuibadilisha mtazamo wa jamii kumhusu. Anaona kuwa ni sharti aonyeshe jitihada na ari ya kupigania haki zake kwa wakati unaofaa.  Nadharia ya ufeministi inazindua mwamko kwa upande wa wanawake kuhusu jinsi anavyojiona na uhusiano wake na watu wengine katika jamii, uhusiano ambao sharti ujengeke katika usawa wa binadamu kitamaduni na kujinsia. Ili kupiga hatua kiuchumi, Nana anafahamu kwamba lazima aweze kudhibiti wakati wake (uk. 109). Anaonyesha ari ya kutaka kuinuka kiuchumi na hata kuwapiku wale waliomtangulia. Anasisitiza kwamba anataka uwe wakati wa kuruka kwake ili awawahi waliomtangulia na waliompita (kur. 110-111).

Nana anadhihirisha mtazamo mpya wa maisha. Juhudi zake ni za kufufua matumaini ya wanawake ambao wamezingirwa katika duru la utamaduni na kizimba cha uoga. Anawahimiza na kuwafunua macho wanawake wachangamkie mabadiliko yenye manufaa kwao. Nadharia ya ufeministi inazindua mwamko kwa upande wa wanawake kuhusu jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine katika jamii. Haya maoni ya Nana

yanadhihirisha mwamko mpya wa mabadiliko yanayotazamia kudhalilisha wakati uliopita na kutilia maanani wakati wa sasa wenye kuleta matumaini mapya katika maisha ya wanaoendelea kudhulumiwa.

Waaidha, Nana anapata mwamko mpya kutokana na vitabu alivyorundikiwa na babake. Vitabu hivi alivisoma Nana chumbani mwake. Vitabu vilimtoa nje ya umbumbu wa kutawa ndani, vikampeleka nje kwa udadisi uliomchemka kichwani kila siku (uk.119).

Faisal anachangia katika kukikuza kipawa cha Nana katika uimbaji. Anamsaidia kuweka msingi katika uwanja wa muziki ambao Nana alinuia kutumia kama njia ya kujipatia riziki. Kupitia kwa Faisal, anapata himizo kwamba anaweza kuimba na kutia fora katika uimbaji wa taarab kama njia ya kujichumia (uk. 54). Nana anagundua kwamba ana kipaji cha uimbaji taarab. Himizo la Faisal linampa matumaini kwamba anaweza kubadili maisha yake kupitia kwa uimbaji. Nana mwenyewe anajihimiza kwamba hakuna ukomo katika kutafuta riziki (uk.129).

Nafasi ya kwanza ya Nana kwenda kutafuta riziki inawadia. Anaenda kujaribu bahati yake katika ‘Hotel Selwa’ kama mwimbaji wa taarab anayeweza kutumbuiza wateja.  Baadaye Nana anakuja kuimarika katika utungaji wake wa mashairi bila ya kuandika, utiaji wa muziki wa papo kwa hapo na uimbaji wenye ufundi usio mfano. Wasimamizi wa Hotel Selwa wangemwajiri na kumlipa laki tatu kwa mwezi. Hata hivyo, Nana anapoteza nafasi hii ya kuajiriwa kwa kuwa heshima zake hazimruhusu kuvaa vazi fupi, kuimba nyimbo zenye mwelekeo wa mpasho, kutamba, kudemka na kukatika. Hivi ni kusema kuwa bado anathamini heshima yake kama mwanamke licha ya kufanya jitihada za kujichumia.

Meneja anamhakikishia Nana kwamba angeongezwa mshahara baada ya muda fulani. Hata hivyo, vikwazo hivyo vinamzuia kukubali kazi hii ila hapotezi matumaini. Baadaye Nana anakuwa na wazo la kuanzisha bendi yake mwenyewe ila changamoto anayokuwa nayo ni pesa. Mawazo ya suala la muziki yanampitikia kama anavyosema msimulizi:

> Kuwa na kikundi chake cha taarab... Na wote hao wangehitaji kulipwa na yeye. Na hilo maana yake nini kama si ule umuhimu wa kuwa na pesa? Pesa za posho na mishahara. Na taarab anayoitaka yeye ni taarab mpya. Taarab itakayomwendeshea maisha na hatimaye kumwezesha kufanya mambo mengi mengine anayotamani kuyafanya mwanamke yeye kwa ajili yake yeye na kwa ajili ya watu wake (uk.157).

Mzinduko wa Nana unamsukuma kutaka kuleta mabadiliko ya kimawazo na ya kitabia. Anataka kujitegemea kwa kila jambo na kutafuta pesa kwa jasho lake mwenyewe. Ili kuleta ufanifu katika biashara yake, Nana anaamua kuzingatia nidhamu kali na kufanya mazoezi ya kuimba. Isitoshe, amepevuka kimawazo. Meneja wa Hotel Crescent anapomwita ‘kimwana,’ analikataa jina hili kwa kuwa hataki mwanamume kumwona tu kama chombo cha kukidhi ashiki za mapenzi jinsi wanavyofanyiwa wanawake wengine. Anamwambia amemwepuka babake kwa matatizo yake, sembuse meneja aking’ang’ania kumwita zaidi kimwana (uk. 164).

Nana ana nia ya kujitafutia riziki kwa kuanzisha bendi yake mwenyewe ya taarab. Anasema:

> Taarab anayotaka kuanzisha ni ya biashara, yeye Mkurugenzi Mkuu (yeye mwenyewe) na msaidizi – mshauri (Faisal), na ofisi zao, na vitengo vya kutolesha video, CD, na DVD, vya watembeza biashara ya taarab yenyewe, vya wahasibu, wakuza biashara hiyo wanaoitwa ‘promoters’, vya redio yake ya FM ya kutangaza vibao vipya na vikonge ili kushindana na vibao vya wengine (kur.196-197).

Kupevuka kwa akili kunamfanya Nana kutambua kwamba anaishi katika dunia ya mashindano. Mashindano yanayolenga kukuza uchumi wa nchi. Nana anaanza kuhesabu mafanikio mengi yanayompa fahari kubwa ya yeye kuwa mwanamke wa kisasa. Anaukumbuka mhadhara alioutoa juu ya mageuzi katika maendeleo ya jamii. Mhadhara huu unazidi kumpa umaarufu kwa wanawake walengwa. Nana anaonyesha upeo wa mzinduko wake wa kiuchumi anapojenga jumba kubwa. Mbali na pesa alizorithi, Nana anadhihirisha uwezo wake katika kuzalisha pesa zaidi kama inavyodhihirika katika usemi ufwatao:

> Ndipo Nana alipojigundua kwamba alikuwa bingwa wa kuzalisha pesa.
> Pesa zilizaa pesa na zilizozalishwa zilizaa nyingine, na nyingine, nyingine,
> na hizo nyingine, nyingine mpaka jambo zima likawa duru la kuzalisha pesa
> tena na tena na nyingine na nyingine (uk.192).

Nana anatambua kwamba ufanisi wa kila mja katika jambo unategemea kiwango chake cha kuweza kuthubutu. Kuthubutu kwake kunamfanya apige hatua kubwa kimaendeleo. Japo anakumbana na vikwazo vingi vikiwemo vizingizio na kunyimwa leseni kadha za biashara, hakati tamaa.

Nana anajenga ghorofa lake kwa ari na vita, kwa nta ya mate kama mchwa wanavyojenga vichuguu vyao (uk.190-191). Ghorofa hili analipa jina ‘Karibu Mwanamke’. Lengo lake kuu ni kuwazindua wanawake wenzake ili waikate minyororo ya udhalimu waliyofungwa nayo na kuanza kuyatazama maisha kwa namna tofauti. Katika ghorofa mbili za mwanzo, anaanzisha duka la vitabu vya kila fani. Ni duka la vitabu pekee lenye uzito nchini. Katika ghorofa ya tatu na ya nne, pana ofisi zote za utawala wa miradi yake ikiwemo ofisi yake yeye mwenyewe Mkurugenzi na ya msaidizi- mshauri wake, Faisal. Ofisi hizi zina masekretari na makarani, wahasibu, mshikafedha na wasaidizi wake na mwendesha ofisi na wasaidizi wake.

Katika ghorofa ya tano kuna ofisi ya kitengo cha Hifadhi ya Watoto na Vijana. Hapa ndipo matatizo yote ya watoto mayatima hutatuliwa. Vilevile matatizo ya vijana wakubwa hutatuliwa humu. Ghorofa ya sita ndipo hutatuliwa matatizo ya wanawake. Hapa panaendeshwa shughuli zote za kumsaidia mwanamke yeyote anayekabiliwa na matatizo ya unyumba, ya kubaguliwa, ya kubakwa, ya magonjwa ya akili ya kukandamizwa, ya magonjwa ya ngono na mengineyo (kur. 190-191). Itagunduliwa kwamba mengi ya masuala haya yana ukuruba mwingi na hali ya mwanamke. Yamesimuliwa hapa ili kuonyesha mchango wa mwanamke katika kuleta utulivu katika jamii iliyojaa fujo za kila aina nyingi yazo zikimwathiri mwanamke.

Nana amefanikiwa na kuwa mwanamke tajiri anayeendesha gari zuri. Anaishi katika nyumba nzuri ambamo mna televisheni, friji na sofa nzuri. Anaishi katika eneo la ‘Mnyonge hajengi’, eneo ambalo wanaishi matajiri pekee katika maisha yanayoweza kulinganishwa na yale ya Ulaya na Marekani. Katika harakati za kuongeza pato lake, Nana hupanda jukwaani kuimba taarab na huongoza kipindi cha ‘Dukuduku’ katika kituo cha televisheni yake. Aidha, ana safari nyingi za kikazi na kibiashara (kur.192-193).

Nana amechorwa kama kielelezo kizuri cha mwanamke aliyejikwamua kutoka katika maisha ya dhuluma hadi kujipata kaneemeka kiuchumi. Hali yake ya kiuchumi ndiyo inabadilisha anavyochukuliwa katika jamii.

Katika *Heri Subira* (2010), Sabra anapitia kila aina za dhuluma ambazo zinampa mzinduko. Mumewe Khalid anampiga, anamtusi licha ya kumwacha pweke nyumbani. Sabra anaonyesha mzinduko wa kiuchumi na nia ya kutaka kujiendeleza. Anaamua kumwacha mumewe Khalid kutokana na udhalimu wake na kwenda kuishi Mayoweni kwa Biti Baraka. Akiwa hapa anamtua Biti Baraka dhiki zote za kuamka mapema ili kutafuta riziki. Anazitwaa biashara zote alizokuwa akizifanya Biti Baraka: biashara ya mahamri, mbaazi na nazi na kahawa alfajiri, biashara ya vyakula adhuhuri na biashara ya vitafunaji na udohoudoho mwingine wakati wa magharibi.

Kila alfajiri akishaondoka kwenye foleni ya maji, hurudi nyumbani kushika kazi ya kuchoma mahamri, kupika chai au kahawa na kukanza moto mbaazi na nazi. Baadaye hupeleka bidhaa hizi uwanjani kuziuza.

Hii inakuwa hatua ya mwanzo ya Sabra kujihusisha katika shughuli za kumwinua mwenyeji wake, Biti Baraka, kiuchumi. Anaonyesha ubingwa wake katika upishi na kuwavuta wateja zaidi mkahawani. Vile vile anakuwa na nia ya kuimarisha biashara hii ili kuzidisha mapato. Msimulizi anasema:

> Sabra alikuwa na nia ya kuimarisha hiyo biashara ya vyakula ili imfaidi
> Biti Baraka apate kidogo cha kujiuguzia (uk.80).

Anamwambia Biti Baraka kuwa anataka ushauri wake kwa sababu angependa kuimarisha hiyo kazi ya biashara (uk.81). Sabra anaonekana kama mwanamke aliyezinduka na yuko tayari kutumia nguvu zake katika kujiinua kiuchumi. Anajitahidi kuimarisha biashara ya mkahawa ili wapate wateja zaidi. Anapendekeza kwamba wanahitaji kuweka mabao ya watu kukalia wanapokula na kuweka redio ili ikiwezekana jamaa wakistaftahi wapate kusikiliza habari (uk.81). Pendekezo hili ni msingi wa kuweza kuinua biashara ya mkahawa.

Biashara ya Sabra inaendelea kuvuma kutokana na huduma bora anazowapa wateja wake. Kuna siku biashara ilinoga hapo uwanjani. Wateja walikuwa wamejazana kwenye eneo la Sabra. Wauzaji wengine walisalia kulia ngoa. Baadhi yao walipata wateja wawili watatu, lakini hakuna aliyempiku Sabra (uk.83). Sabra anamwomba Heri waungane ili washughulikie biashara kwa pamoja. Naye Biti Baraka anamuunga mkono ombi hili.

Bidii ya Sabra katika biashara inafanya hali yao ya maisha kuimarika. Sasa kochi wanalokalia ni safi kiasi. Nyumba nzima imesakafiwa. Kuta za ndani zimetandazwa zege. Vitu vyote vya zamani vimeondolewa. Kabati la vyombo lilikuwa jipya na juu yake lilikuwa na karabai (uk.111). Ni bayana kwamba Sabra aliyekiuka vizingiti vya utamaduni wa jamii kwa kumwacha mumewe wa kulazimishwa sasa yuko huru. Nadharia ya ufeministi inanuia kuwasaidia wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Dhuluma alizopitia akiwa kwa Khalid zilimfanya azinduke na kuwa na mtazamo mpya wa maisha.

Katika sehemu hii, tumedhihirisha namna mwanamke alivyozinduka na kubadilisha hali yake ya kiuchumi. Anavuka mipaka na kuondoa vikwazo alivyowekewa na mwanamume kwamba yeye ni duni na kwamba mahali pake ni jikoni tu. Anaonyesha kwamba anao uwezo wa kuibadilisha jamii yake kiuchumi kutokana na juhudi zake mwenyewe.

### 3.2 Mzinduko wa Kimapenzi

Wanawake wanapokumbana na dhuluma ya kuozwa kwa lazima, huchochewa kiakili na kupata mzinduko wa kimapenzi. Mzinduko wa kimapenzi hutokea pale wanawake hawa wanapoasi itikadi za kitamaduni na kuamua kujichagulia waume wao wenyewe. Hatua hii huwafanya kuishi maisha mazuri kwa kuwa ndoa zao sasa huwa zimejengwa kwenye msingi wa mapenzi wala sio kulazimishwa.

Katika *Nyuso za Mwanamke*, Nana anadhihirisha mzinduko wa kimapenzi. Tangu awali hakupenda ndoa ya lazima. Anaamini kwamba ndoa ni zao la mapenzi na iwapo mapenzi hayapo basi ndoa bila shaka haitafanikiwa. Nana anaikataa mikatale ya mapenzi ya kulazimishwa. Anafufua matumaini ya kuwepo kwa mapenzi ya dhati ambayo ni ya waziwazi na bila sababu ya kidunia. Anasema:

> A-a mapenzi ya mwili hayamo ndani ya moyo wangu. Na kwa nini mapenzi
> lazima yawe ya mwili katika jamii hii? Hapana, haya yangu labda ni
> mapenzi ya roho – mapenzi ya kumpenda mtu ambaye ninadhani
> mwema, ninayempenda bila sababu ya waziwazi na bila sababu ya kidunia (uk.113).

Nana anamkataa Dusa, mwanamme tajiri aliyechaguliwa na wazazi wake awe mwenzi wa kuishi naye milele. Siku ya sherehe ya kuadhimisha miaka ishirini na moja ya Nana kuzaliwa, Dusa anaaibishwa. Dusa amejaribu kumvuta kwa tamasha kadha bila mafanikio. Isitoshe, Nana analikataa gari bichi, aina ya Volvo, alilonunuliwa na Dusa aliposherehekea kuzaliwa kwake (uk.45).

Uasi huu wa Nana unazua hasira ambayo inamsababishia kichapo cha babake. Baadaye, Nana anakutana na Amour (mwanawe Faisal). Ari ya mahaba yanapobubujika moyoni mwake na kumsakama, anajasiria kumwambia Amour. Nana ndiye anayepanga na kumwalika Amour katika mkahawa wa Samrah. Anajikwatua kuliko afanyavyo akienda safari za kikazi hata anapojitokeza kwenye televisheni. Hisia za mapenzi kwa Amour zinamnyonga hadi kumlazimisha kuanzisha na kuongoza mazungumzo yake naye. Anaenda kinyume na kaida za kitamaduni zinazomtarajia mwanamme kuanzisha ngoma ya mapenzi.

Nana anaonekana kukiuka kaida za mapenzi zinazomtarajia mwanamume kuanzisha mazungumzo ya mapenzi hasa katika jamii za Kiafrika. Licha ya kushauriwa dhidi ya ndoa, anakata kauli na kuolewa na Amour. Kupitia kwa Nana, mwanamke anaonekana kama kiumbe aliyekata pingu ya udhibiti wa kitamaduni kuhusu mapenzi na ndoa. Wanajipa uhuru wa kuchagua wachumba na waume zao. Wametanabahi kuwa ndoa ya kudumu hutokana na mapenzi ya dhati. Wako tayari kuyafia mapenzi ya dhati ya mioyo na nafsi zao. Hivyo wanafaulu kuleta mapinduzi katika taasisi ya ndoa.

Hatua ya Nana ya kuolewa na Amour inasaidia katika kufufua matumaini yake na ya wanawake wengine ambao wanalazimishiwa ndoa na wachumba pamoja na wale ambao wanahofia kuwa huenda utamaduni ukawalazimishia wachumba. Nana sasa amekuwa mke wa Amour, mwanamume ambaye anampenda kwa moyo wake wote na ambaye ni chaguo lake mwenyewe (uk. 293).

Nana anafurahia ndoa yake na Amour. Awali alihisi kama kwamba amepungukiwa kitu japo mali alikuwa nayo. Kuja kwa Amour maishani mwake kunamfanya ajihisi mwanamke kamili. Anaamini kwamba ndoa ni kitu kizuri iwapo wahusika wote wawili wameridhiana.

Wanawake wengine kama Bimkubwa na Shemsa, wanafuata nyoyo zao kwa kiasi cha kugura ndoa zao za lazima walizosukumiwa na wazazi wao. Hawajali kidole cha jamii kitakachowaelekezea lawama. Bimkubwa aliwaambia wazazi wake waziwazi kuwa hakumtaka wala hakumchagua Bw. Hila. Alikataa kuozwa kwa Bw. Hila. Naye alijitolea mhanga kumpenda mchumbawe, Faisal, kwa dhati. Hata hivyo, alikuja kuozwa kwa lazima.

Kwa upande mwingine, Shemsa anawatangazia wazazi wake kuwa hakumpenda wala kumuenzi Sadiki. Mwanamke anaonyesha kuwa ana uhuru wa kimapenzi ambao unamwezesha kujichagulia mchumba kwa wakati ufaao. Hivyo anaikata minyororo iliyomfunga.

Katika *Heri Subira* (2010), Sabra anapata mzinduko wa mapenzi anapoamua kwamba hataendelea kuishi na mumewe Khalid. Ndoa kati yake na Khalid ilikuwa ya kulazimishwa wala haikujengwa kwenye msingi wa mapenzi na uaminifu. Sabra anajaribu kuvumilia dhuluma anazofanyiwa na Khalid hata inapofikia wakati ustahimilivu wake unaisha. Anaamua kuondoka kwenda Mayoweni kwa Biti Baraka. Dhuluma zinamfanya Sabra awe na ujasiri. Ujasiri wa kuweza kuomba talaka kwa mumewe Khalid. Anasema katika barua aliyomwachia Khalid mezani kwamba:

> Ninakuomba jambo moja tu kwa hisani yako, ninataka talaka yangu.
> Sijui nitapataje habari ya talaka, lakini tutayajua hayo huko twendako.
> Pengine hii ndoa si heri yetu sote (uk.74).

Nana anadhihirisha kwamba yeye kama mwanamke amezinduka na kuikata minyororo aliyofungiwa nayo katika ndoa iliyojaa unyanyasaji. Anapiga hatua muhimu ya kuomba talaka yake kinyume na desturi ya jamii. Maoni ya Nana yanashabihiana na ya Beauvoir (1949), ambaye anashambulia asasi za jamii zinazochangia ukandamizaji wa mwanamke zikiwemo ndoa, utamaduni na dini. Akiwa kwa Biti Baraka, Sabra anaandika barua kumkumbusha Khalid masuala ya talaka. Ujumbe katika barua yake unabainisha kwamba Sabra hayuko tayari kuridhiana na Khalid. Anachangamkia suala la ndoa yake kufikia tamati.

Alipotoka nyumbani kwa Khalid, Sabra hakujua kwamba siku nyingine atakuja kuotewa mche wa mapenzi moyoni. Hata hivyo ameanza kuwa na hisia za mapenzi kwa Heri. Anajijasiria kumuuliza Heri sababu iliyomfanya asioe (uk.96). Heri anapomjibu kwamba hajapata mzuri wa kumuoa, Sabra anamhimiza kwamba akitafuta basi atapata. Mazungumzo haya yanadhihirisha hisia tofauti na zile walizokuwa nazo vijana hawa hapo awali. Ndiyo yaliyoiotesha mbegu ya uhusiano wa wawili hao kuandama mkondo mwingine. Walianza kuwa na ukuruba zaidi. Wakiwa kazini, kila walipopata nafasi walizungumza mambo ya unyumba tangu raha hadi karaha zake (uk.97).

Kadri siku zinavyopita ndivyo Sabra anazidi kumpenda Heri. Tofauti na penzi lake la awali, huyu sasa ni chaguo lake la moyoni. Mapenzi yakawa yanambubujika. Sabra anaamua kuvunja miiko ya utamaduni wa jamii kwamba mvulana ndiye anakuwa wa kwanza kuposa. Anakuwa wa kwanza kumweleza Biti Baraka kuhusu mche wa mapenzi ambao kwa muda sasa ulikuwa umewaotea mioyoni (uk. 97).

Japo inamwia vigumu kuanza mada hiyo kwa mwenyeji wake kwa hofu kwamba angemkasirisha, Sabra anapata ujasiri hatimaye (uk. 98). Anaupata ujasiri wa kusema mambo haya kwa kuwa ni mwanamke ambaye amebadilika. Amebadilika kimawazo na kimtazamo. Biti Baraka, kwa upande mwingine anashangazwa na uamuzi wa Sabra hasa akizingatia kuwa kuja kwake Mayoweni kulisababishwa na jambo kama hilo, yaani dhuluma katika ndoa. Hata hivyo anaamua kutopinga uamuzi wa Nana. Nadharia ya ufeministi inakuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Sabra anaendelea kusema:

> Bibi, samahani kwa kauli yangu hiyo. Najua si kawaida kwa mwanamke wa kikwetu...Tumezungumza. Mimi na yeye tunataka ridhaa yako kwanza, kisha nipeleke ujumbe kwa wazazi wangu. Wakubali wasikubali mimi nimeshaamua (uk. 99).

Mzee Fauz kwa upande mwingine anakataa kuridhia suala la Sabra kutaka kuolewa na mume mwingine. Hata hivyo, Sabra anatambua kwamba ana haki ya kujichagulia mume anayempenda. Anamkaidi babake na kuolewa na Heri. Mapenzi ya Sabra kwa Heri hayawezi kuzuiliwa hata kama angekosa baraka kutoka kwa babake mzazi. Kinachomridhisha ni kwamba amempata mume aliye na sifa alizozihitaji:

> Sabra alimpenda Heri kwa dhati. Hakuzingatia rangi ya ngozi yake. Alichoridhia ni kuwa Heri alikuwa binadamu. Alikuwa mtu na utu. Ziada ya hayo, alikuwa mswahilina. Aliiweka ibada mbele na hivyo akawa na hulka ya kumvutia kiumbe yeyote aliyekutana naye. Alikuwa tayari kumfaa yeyote kwa vyovyote vile. Hakuwa na kipato kikubwa, lakini alikuwa na mkono wa kutoa (uk.110).

Sabra sasa anafurahia ndoa yake ya pili. Ndoa ambayo ni zao la mapenzi ya dhati kati yake na Heri wala sio kulazimishwa na wazazi. Ndoa yake ya chuo cha pili haikuwa na mambo mengi. Nikaha ilifungwa ikashuhudiwa na watu wachache tu. Kutoka hapo ikawa ni yeye Sabra, mamezaa wake na mumewe tu (uk.111).

### 3.3 Mzinduko wa Wanawake na Uwezeshwaji wa Kiswahili

Kuzinduka kwa mwanamke ni hali inayotia jamii pana changamoto kuhusu namna ya kuhusiana naye katika nyanja mbalimbali. Kadri siku zinavyoendelea kusonga ndivyo mwanamke wa kisasa anavyoendelea kupata nafasi ya kushiriki katika mambo mbalimbali yanayohusu maisha yake na hali ya jamii kwa jumla. Wanawake wengi wameshiriki katika uwezeshwaji wa Kiswahili kwa kukifanyia tafiti mbalimbali za kitaaluma katika eneo la fasihi na isimu. Wengine wameweza kushiriki katika maadishi ya kazi za sanaa. Baadhi ya tafiti na maandishi haya kwa Kiswahili yameangazia njia za kuboresha maisha ya mwanadamu kwa kutumia malighafi na rasilmali zilizopo. Aidha, wanaendelea kutoa maandishi na tahakiki zinazohusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuimarisha mahusiano ya watu na kuendeleza jamii kiuchumi.

### 4.0 Hitimisho

Makala hii imejadili mzinduko wanaopata wanawake baada ya kudhulumiwa. Wanawake waliorejelewa katika makala hii wanaonyesha mwamko mpya wa kukataa unyanyasaji na badala yake kupigania haki zao. Athari zinazotokana na kukandamizwa kwao zinajitokeza kama shime inayowasukuma kufungua ukurasa mpya wa maisha yao.

Utafiti huu umethibitisha kwamba kwamba mwanamke wa Kiafrika anakabiliwa na dhuluma kutoka jamii inayotawaliwa na ubabedume. Hata hivyo dhuluma wanazopitia wanawake zinawapa mzinduko wa kiuchumi na kimapenzi. Wanakataa kuishi kwa utegemezi wa wanaume na kuziasi taasisi dhalimu za kijamii zinazowakalia na kuwafungia katika ngome kiuchumi na kimapenzi. Wanawake wamepata uhuru wa kuwa mjasiriamali na kuwekeza katika miradi inayozalisha faida na vilevile kujiamulia hatima yao katika masuala na mapenzi na ndoa. Hivi ni kusema kuwa mwanamke ametambua kuwa yeye ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii yake.

Nadharia ya Ufeministi inatambua kwamba mwanamke wa Kiafrika anahitaji kwanza kuelewa jamii kandamizi anamoishi. Ujuzi huu humwezesha kupata kujielewa mwenyewe, kujitathmini, kujiumbua na kushirikiana na wanawake wengine katika kujiweka nafasi anayostahili katika jamii ya kisasaleo. Kutokana na mchango mkubwa wa wanawake katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Kiswahili, ni bayana kuwa mzinduko wao utawasaidia kuiwezesha lugha ya Kiswahili kutumika kama wenzo wa maarifa katika sekta mbalimbali**..**

### REFERENCES

*Babu, O. (2010). Heri Subira. Nairobi: Oxford University Press.*

*Beauvoir, S. (1949). The Second Sex. London: Pan Books Publishers.*

*Corrin, C. (1996). Women in a Violent World. Edinburgh: Edinburgh University Press.*

*Disch E. (2009). Reconstructing Gender: A Multicultural Anthology. Newyork: Mc*

*Freeman, J. O. (Ed) (1975). Women: A Feminist Perspective. California: Mayfield Publishing Company. Graw- Hill Publishers.*

*Greer, G. (1971). The Female Eunuch. New York: McGraw.*

*Hynes, H. P. (1989). Reconstructing Babylon: Essays on Women and Technology. London: Earthsan.*

*Kimani, C. W. (2003). 'Swala la Dhuluma dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Isiyochapishwa).*

*Lugano, R. S. (1989). "Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.*

*Matteru, M. O. B. (1992). 'The Image of the Woman in Tanzania Oral Literature,' makala katika Kiswahili vol. 49/2 TUKI. Dar es Salaam.*

*Mbogo, E. (1990). 'Kwenye Ukingo wa Thim.' makala katika Jarida la Kiswahili K. J. No.1. Educational Services Centre, Dar es Salaam.*

*Mohamed, S. A. (2010). Nyuso za Mwanamke. Nairobi: Longhorn Publishers.*

*Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makahaba katika vitabu vya Said Ahmed Mohamed." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Isiyochapishwa)*

*Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.*

*Wegesa, B. B. (1994). 'Mwanamke katika Tamthilia za Ebrahim Hussein.' Tasnifu ya M. Phil, Chuo Kikuu cha Moi. (Isiyochapishwa).*

*Wollstonecraft, M. (1792). A Vindication of the Rights of Women. Uk: Forgotten Books.*